# BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET)

## TAARIFA KWA UMMA

### MATOKEO YA UCHAGUZI WA UDAHILI KUPITIA MFUMO WA UDAHILI WA PAMOJA (CAS) KWA KOZI ZA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KWA MWAKA WA MASOMO 2026/2027 - AWAMU YA PILI

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linautaarifu umma kuwa matokeo ya uchaguzi wa awamu ya pili kwa waombaji wa programu za Afya na Sayansi Shirikishi kwa mwaka wa masomo 2026/2027 yametangazwa rasmi leo tarehe 4 Septemba, 2026.

Jumla ya waombaji **16,504** walikamilisha maombi ya udahili, kati ya hao waombaji **12,249** walikuwa na sifa kwenye programu walizoomba na waombaji **4,255** hawakuwa na sifa kwenye programu walizoomba.

Jumla ya waombaji **9,757** wamechaguliwa kujiunga kwenye vyuo vinavyotoa programu mbalimbali za Afya na Sayansi Shirikishi ambapo wanawake ni **4,995 (51.19%)** na wanaume ni **4,762 (48.81%)**. Waombaji **684** walichaguliwa kwenye vyuo vya Serikali na waombaji **9,073** katika vyuo visivyo vya Serikali.

NACTVET Makao Makuu, Jengo la Kambarage - Ghorofa ya 7
S. L. P 387, Dodoma | +255 736 310311 | info@nactvet.go.tz | www.nactvet.go.tz

Aidha, waombaji wenye sifa ambao hawakuchaguliwa kutokana na ushindani katika programu na vyuo walivyoomba, wanashauriwa kuomba kujiunga katika vyuo vyenye nafasi katika dirisha la awamu ya tatu kupitia Mfumo wa Udahili wa Pamoja.

Waombaji wote wanaweza kuangalia matokeo ya uchaguzi kupitia tovuti ya Baraza **(www.nactvet.go.tz)** kwa kubonyeza **CAS Selection Results 2026** kwa ajili ya kupata taarifa zaidi.

Baraza linautaarifu umma kuwa dirisha la awamu ya tatu litakuwa wazi kuanzia leo tarehe **4 hadi 26 Septemba, 2026** na matokeo ya uchaguzi yatatolewa tarehe **9 Oktoba,2026.**

Aidha, wale wanaohitaji kubadilisha programu au chuo, dirisha la uhamisho litakuwa wazi kuanzia tarehe **4 hadi 26 Septemba, 2026**, hivyo watumie dirisha hili kukamilisha maombi hayo kupitia tovuti ya Baraza kwa kubonyeza kwenye akaunti yake aliyotumia kuomba na kuchaguliwa.

**IMETOLEWA NA:**
**Kitengo cha Mawasiliano na Masoko**
**NACTVET**
**04/09/2026**